**HOTUBA YA MHE.HAROUN ALI SULEIMAN, WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA KATIKA MKUTANO NA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU MAADHIMISHO YA WIKI YA MSAADA WA KISHERIA-2023**

**UKUMBI: WIZARA MAZIZINI – ZANZIBAR**

**TAREHE: 15/07/2022**

Naibu Katibu Mkuu, Afisi ya Rais,Katiba,Sheria,Utumishi na Utawala Bora;

Mkurugenzi wa Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria;

Watendaji wa Wizara;

Afisa Program Mwandamizi kutoka LSF;

Waandishi wa habari.

**Assalam alaikum.**

Kwanza kabisa, napenda nichukue nafasi hii adhimu kwa kuweza kumshukuru Allah kwa kutujalia afya njema ya kukutana siku ya leo kwa lengo la kupeana taarifa juu ya maadhimisho ya Wiki ya Msaada wa Kisheria kwa mwaka 2023 ambayo yanaratibiwa na Ofisi ya Rais- Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kupitia Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria kwa kushirikiana na Shirika la Legal Service Facility (LSF).

Aidha, napenda kuwashukuru Shirika la LSF kwa kushirikiana na Ofisi hii katika kuhakikisha kuwa wananchi wetu wa Zanzibar wanapatiwa msaada wa kisheria popote pale walipo. ***Ahsanteni, sana.***

**Ndugu waandishi wa habari,**

Kama tunavyoelewa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawajali sana wananchi wake hasa katika kuhakiksiha kuwa inazungukwa na jamii yenye ustawi mzuri uliomarika katika kila nyanja ya maisha pamoja na kuhakikisha wananchi wake hususan wanyonge na wasiojiweza wanapatiwa msaada wa kisheria bila ya usumbufu wowote. Hivyo, lengo kuu la Wiki ya Msaada wa Kisheria ni kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa jamii yetu inayotuzunguka.

**Ndugu waandishi wa habari,**

Kauli mbiu ya maadhimisho ya wiki ya msaada wa Kisheria kwa mwaka 2023 ni ***"MAZINGIRA WEZESHI KWA WATOA MSAADA WA KISHERIA NI DARAJA LA UPATIKANAJI HAKI"***.

Kauli mbiu hii ina lengo la kuhakikisha kunakuwepo na mazingira mazuri ya utoaji msaada wa kisheria kwa watoaji wa msaada wa kisheria.

Bado kuna changamoto kubwa kwa watoaji wa msaada wa kisheria ikiwemo uhaba wa bajeti na upatikanaji wa Ofisi za kudumu zenye mazingira mazuri ya utoaji wa msaada wa kisheria.

Aidha, ifahamike kuwa watoaji wa msaada wa kisheria hufanya kazi zao kwa kujitolea, uzalendo na jitahada kubwa katika kuhakikisha wananchi wasio na uwezo, watu wenye ulemavu na watu wa makundi maalum wanapatiwa msaada wa kisheria hivyo, kufanikiwa kwa jitahada zao inategemea na uwepo na mazingira wezeshi ikiwemo mashirikiano kwa jamii, upatikanaji wa rasilimali fedha za kutosha, vitendea kazi na kadhalika.

Ni matarajio yetu kwa kauli mbiu hii kuwa ni chachu ya upatikanaji wa mazingira mazuri kwa watoaji wa msaada wa kisheria.

**Ndugu waandishi wa habari,**

Maadhimisho haya ya Wiki ya Msaada wa Kisheria yatajumuisha shughuli mbali mbali kwa upande wa Unguja na Pemba. Shughuli zitakazofanyika ni kama zifuatazo: -

- Utoaji wa elimu kwa wananchi kupitia redio na TV, hii itakuwa ni kampeni maalum kupitia vyombo vya habari katika kuwafikishia wananchi taarifa sahihi juu

ya maadhimisho haya na upatikanaji wa msaada wa kisheria Zanzibar.

- Kona ya Msaada wa Kisheria, hii itafanyika katika kuyapitia makundi mbali mbali kama vile vijana, watoto wanaojisuhulisha na michezo mbali mbali na kuwapatia msaada wa kisheria. Pia shughuli hii itajumuisha mjadala wa uzoefu wa masuala ya msaada wa kisheria.
- Ziara ya kutembelea vyuo vya mafunzo kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria.
- Shughuli ya usafi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.
- Bonanza la Msaada wa Kisheria lenye kuhamasisha katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

Vile vile, Taasisi za Watoa msaada wa kisheria zilizopo katika kila Wilaya na maeneo mbali mbali nazo zitatoa msaada wa kisheria kwa wananchi kupitia shughuli mbali mbali.

**Ndugu waandishi wa habari,**

Napenda niwaeleze kuwa siku ya Jumamosi tarehe **22/07/2023** itakuwa ndio maadhimisho yenyewe ya Wiki ya Msaada wa Kisheria ambayo yatafanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idris Abdul Wakil- Kikwajuni.

Siku hii Mgeni Rasmi tunatarajiwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Aidha, shughuli hii itahudhuriwa pia na Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri, Wakuu wa Vikosi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mahakama, Watendaji mbalimbali wa Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali, Wawakilishi kutoka Mashirika ya Maendeleo, Watendaji wa Ofisi ya Rais, Katiba,Sheria,Utumishi na Utawala Bora, Watendaji wa LSF, watoaji msaada wa kisheria, wataka huduma, na waandishi wa habari.

Vile vile, tunatarajia shughuli hii kuwa na tukio la Utoaji wa Tuzo za Mwaka za Kitaifa za Watoaji Msaada wa Kisheria Zanzibar.

**Ndugu waandishi wa habari,**

Niwaombe kushirikiana nasi katika kuhakikisha wananchi wetu wanapata taarifa sahihi juu ya upatikanaji wa msaada wa kisheria katika nchi yetu ya Zanzibar. Ni imani yangu kuwa mna nguvu kubwa ya kuweza kuwafikia wananchi kupitia uweledi wa taaluma yenu, hivyo ni vyema mkalifanikisha hili ili baada ya maadhimisho haya tukija kufanya tathmini basi tuwe tumewafikia wengi na

faida iliopatikana kutokana na msaada wa kisheria uliotolewa.

**Mwisho,**

Napenda kukupongezeni kwa kuweza kujumuika nasi katika siku ya leo na pia ushirikiano wenu kwa Ofisi ya Rais,Katiba,Sheria,Utumishi na Utawala Bora katika shughuli mbali mbali, naomba muendelee pia kushirikiana bega kwa bega na Ofisi yetu kwa kuhakikisha wananchi wanaielewa vizuri na hapo ndipo itakapokuwa nafasi yao kuwajua wale watoa huduma za msaada wa kisheria na kuweza kuwatumia.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza**